# MAELEZO NA MASHARTI YA MKOPO BINAFSI WA FEDHA

Maelezo na masharti yanayorejewa humu yanaeleza haki na wajibu wa mwombaji na Benki kuhusiana na mshahara/mkopo (ambao utarejewa hapa kama "mkopo"). Mkopo unaweza kupatikana mapema ama kupitia (i) maombi ya maandishi (ii) Huduma ya Data ya Ziada Isiyo Rasmi (USSD) maombi (*150*29#) (iii) maombi ya simu ya Stanbic na (iv) benki kwa intaneti.

**Tafsiri**

"**akaunti**" maana yake ni akaunyi ya mkopo iliyofunguliwa katika vitabu vyetu kuhusiana na mkataba huu.

"**mkataba**" maana yake ni maombi ya mkopo wa fedha , fomu nyingine za maelezo ya ziada,maelezo na masharti haya na maelezo yote ya malipo, barua, taarifa na viambatisho vilivyopo.

"**mwombaji," "mkopaji," "wewe" au "yako**" ina maana ya mtu anayeomba mkopo wa fedha.

"**benki","sisi", au "yetu"** ina maana ya Benki ya Benki ya Stanbic Tanzania Limited (Usajili Na. 22443), kampuni ambayo imeandikwa rasmi na ukomo wa dhima kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni Na.12 ya 2002 ya Tanzania Bara na kupewa leseni chini ya Sheria ya Benki na Asasi za Kifedha 2006 (Sheria Na. 5 ya 2006, kama ilivyorekebishwa mara kwa mara) na/au warithi wa hakimiliki au wahawilishwa.

"**siku za kazi**" ina maana ya siku, isipokuwa Jumamosi, Jumapili na likizo ya umma Tanzania.

"**akaunti ya hundi**" ina maana ya akaunti hai ambamo amana zinaweza kuwekwa na kutolewa kwa kutumia hundi, bili, maidhinisho ya malipo au njia zetu za huduma binafsi.

"**Ofisi ya Taarifa za Mikopo** ("CRB" ina maana ya ofisi ya taarifa ya mikopo iliyopewa leseni na Benki Kuu ya Tanzania kuthibitisha taarifa yoyote iliyotolewa na Mkopaji.

"**Ukomo",** "ukomo uliokubaliwa",

"**Ukomo wa mkopo" au" ukomo wa mkopo uliopunguzwa** "ina maana ya kiasi cha mkopo ambacho kinapatikana kwa matumizi yako kwa mujibu wa mkataba huu.

"**mkopo**" ina maana ya kiasi ambacho tumekubali kukukopesha kwa mujibu wa mkataba huu,

"tarehe ya malipo" au "tarehe husika" ina maana ya tarehe inayohusika kwa malipo ya kiasi chote kinachotakiwa kulipwa, "na

"**ulipaji**" ina maana ya malipo uliofanya kwetu kulipa mkopo wako.

**1. Ulipaji**

1.1 Mkopo unalipwa inapodaiwa au ulipaji na utalipwa na wewe katika tarehe itakayoelekezwa kwako katika jedwali la ulipaji, lakini kwa vyovyote vile sio baada ya siku 30 (thelathini) kutoka tarehe ya malipo.

1.2 Malipo yako yote, yawe ya kiasi kikuu, ada, gharama,tozo au vinginevyo

yatalipwa kwa ukamilifu, bila kukata deni au madai kinzani, na kuwa huru kutokana na makato, kodi au vinginevyo.

1.3 Nyakati zote wajibu uko kwako kuhakikisha kuna fedha za kutosha kufanya ulipaji kama ilivyoainishwa kwenye tarehe kwenye jedwali la ulipaji lililoambatishwa hapa.

1.4 Ikiwa utashindwa kulipa kima cha chini cha malipo ya kila mwezi kwa siku iliyopangwa kwa ukamilifu au kwa vyovyote, tunaweza kuamua kiasi hicho au, kadri iwavyo, kuhamishwa kutoka akaunti yako yoyote iliyonasi na maelekezo ya upungufu wa malipo yaliyokuwepo yatachukuliwa kurekebishwa ipasavyo.

1.5 Unaturuhusu kukata kutoka kwenye akaunti yako iliyo nasi siku yoyote ambayo tunaona lazima kukusanya ulipaji unaodaiwa.

1.6 Unaweza kulipa deni mapema,na hutatozwa kwa ulipaji huo wa mapema.

1.7 Malipo yote yaliyofanywa chini ya mkopo huu yataingizwa na sisi siku ya upokeaji kukamilisja deni kuu ambalo liko na gharama yoyote na ada kwa mujibu wa mwongozo wa ushuru.

**2. Upangaji bei**

2.1 Mkopo utatozwa ada ya uchakataji 5% (asilimia tano) ya mkopo ambayo italipwa katika tarehe ya ulipaji deni.

2.2 Ikiwa kiasi chochote unachotakiwa kulipa katika mkopo wowote hakitalipwa unapotakiwa, kiasi hicho kitatozwa riba ya ukiukaji kiasi cha 10% (asilimia kumi) kwa mwaka, kuanzia tarehe ambapo kiasi hicho kilitakiwa kulipwa hadi tarehe ambapo kitalipwa.

2.3 Riba ya adhabu inayotakiwa kulipwa kwenye mkopo:

2.3.1 itakokotolewa kwa msingi wa mwaka wa siku 365 kwa mikopo kwenye shilingi za Kitanzania na mwaka wa siku 360 kwa mikopo ya fedha za kigeni bila kujali kama mwaka unaohusika ni mwaka mrefu.

2.3.2 ongezeko siku hadi siku; na

2.3.3 itakokotolewa kwa bakaa inayodaiwa chini ya uwezeshaji mkopo bila kujali kama bakaa hilo linaweza kuongezeka kwa kukatwa na riba;

2.3.4 kukatwa kwenye akaunti yako ya mkopo kwa malimbikizo ya mwezi.

**3. Mabadiliko katika Mazingira**

Tunaweza mara moja kurekebisha mfumo wa uwekaji bei wa mkopo ikiwa kuna mabadiliko yoyote katika sheria, sheria kuu, kanuni, uamuzi, maelekezo, sera au kama tukio kama hilo ambalo tunalazimika kutekeleza na kusababisha ongezeko katika gharama kwetu. Tutakuarifu kwa njia tofauti, hii ni pamoja lakini sio pekee, vyombo vya habari, taarifa kwenye mashine za kutolea pesa na ndani ya matawi yetu, na

njia nyingine ambazo tutaona zinafaa mara kwa mara.

**4. Cheti cha kiasi kinachodaiwa**

Kiasi cha deni lako kwa wakati wowote na ukweli kwamba kudaiwa huko (pamoaj na riba yoyote na kima ambacho na kipindi ambacho riba inakokotolewa kimewadia, kinaweza kuamuliwa na kuthibitishwa kwa cheti kinachoelezea hivyo kilichotiwa saini na afisa muidhiniwa wa Benki, ambaye uteuzi na mamlaka yake kutia saini hayahitaji kuthibitishwa. Cheti hicho kitakuwa ithibati ya kutosha ya yanayosemwa ndani yake.

**5. Mapato**

5.1 Unakubali kuwa na akaunti ya hundi na sisi ambamo mshahara wako au mapato yataingizwa.

5.2 Unaruhusu bila pingamizi kutoa katika akaunti ya hundi malipo ya kila mwezi pamoja na ada za benki na kiasi chochote kilichobaki kwenye mkopo. Maelekezo hayo yatabaki kwa muda wote wa mkopo na mpaka tuamuru kuondolewa.

5.3 Katika kipindi cha mkopo huu unathibitisha kuwa hutatoa maelekezo yoyote tofauti kuhusu malipo bila ya ruhusa yetu ya maandishi.

5.4 Ikiwa Mabadiliko Makubwa Muhimu yametokea. Benki ina haki ya kupitia masharti ya mkopo (nyenzo) kubadilisha mkopo (nyenzo) kuwa mkopo utakaolipwa unapodaiwa au kutaka dhamana ya fedha kwa kiasi chote cha deni la Mkopaji pamoja na dhima inayoweza kutokea.

Katika kipengele hiki “Mabadiliko Hasi Makubwa yatakuwa na maana ya mabadiliko katika hadhi ya kipato ya Mwombaji au jambo lolote ambalo kwa maoni ya Benki ni muhimu kwa dhima ya mkopo kwa Mkopaji.

**6. Kusitisha na kutengua**

6.1 Kiasi cha mkopo kinaweza kusitishwa na/au kutenguliwa na sisi kwa busara yetu wenyewe kwa taarifa ya maandishi kwako, ambapo mkopo utaondolewa hivyo kutakiwa kulipwa.

6.2 Yote au sehemu ya ukomo wa mkopo au ukomo wa mkopo uliopunguzwa (ikiwa inahusika) inaweza kuondolewa na sisi kwa taarifa ya maandishi kwako, iwe umekiuka au la, ambapo kiasi chote kilichozidi mara moja kitatakiwa kulipwa.

**7. Ukiukaji**

7.1 Tukio la ukiukaji kwenye mkopo litatokea iwapo:

7.1.1 unakiuka maelezo na masharti yoyote ya mkopo wako au mkataba mwingine kati yako na sisi na ni sahihi kurekebisha ukiukaji ndani ya siku 7 (saba) baada ya taarifa ya maandishi kutolewa kwako ili utekeleze; au

7.1.2 unashindwa kulipa mkopo ndani ya siku 30 (thelathini) kuanzia siku ya malipo kwa mujibu wa mkataba huu; au

7.1.3 ikiwa Benki itakuwa na maoni kwamba kumekuwa na hali mbaya yako ya kifedha au mwenendo wa shughuli za akaunti yako;

7.1.4 maelezo au udhamini vilivyofanywa kuhusiana na mkopo wako au nyaraka zozote zilizotolewa na wewe, kwa maoni yetu, sio sahihi, hazijakamilika au kupotosha; au

7.1.5 mashauri yanaanzishwa kukutangaza kuwa umefilisika au amri ya mpito au ya mwisho imepitishwa kutaka kuwa umefilisika, au makubaliano au mipango kati yako na wadai wako imetelekezwa au imewadia; au

7.1.6 hati ya utekelezaji amri imetolewa na mahakama yenye uwezo kukamata mali yako yoyote;

7.1.7 unakoma kuwa mfanyakazi wa kampuni au asasi;

7.1.8 mshahara au mapato hayapitishwi kupitia Benki kutokana na sababu yoyote;

7.1.9 makubaliano au mpango wowote kati yako na wadai wako yanatekelezwa;

7.1.10 kwa jumla unafanya au kuacha kufanya kitu chochote ambacho kinaweza kuathiri haki zetu kuhusiana na saini au kusababisha sisi kupata hasara au madhara; au

7.2 Ikiwa ukiukaji unatokea kama ilivyotegemewa kwenye aya 7.1, Benki itakuwa na haki bila kuathiri haki nyingine au nafuu zinazopatikana kwa Benki, kufuta mkopo na kudai ulipaji wa haraka wa bakaa iliyobaki kuanzia mara au katika tarehe iliyotajwa kwenye taarifa. Ikiwa mkopo unafutwa kiasi chochote ambacho kimebaki kinatakiwa kulipwa kwa Benki:

7.2.1 mara moja ikiwa imeelezwa kwenye taarifa; au

7.2.2 katika tarehe iliyotajwa kwenye taarifa.

7.3 Kwa mujibu wa ukiukaji kama ilivyotajwa katika aya ya 7.1.1 na 7.1.2, inakubalika hapa kwamba jina la mkopaji na maelezo kamili yanaweza kutolewa na benki kwa Wakala wa Kumbukumbu za Mikopo kwa usambazaji kwa mkopeshaji ambaye anaweza kutumia taarifa kama hiyo kutathmini uwezo wa mkopaji kwa matumizi ya biashara zao baada ya taarifa ya maandishi ya siku 28 (ishirini na nane) kuanzia siku ya ukiukaji.

**8 Makato Deni na Ulipaji**

8.1 Ikiwa kutatokea ukiukaji, Benki inaweza, wakati wowote bila ya taarifa ya ziada kwako, na bila kujali kiasi au jambo lolote jingine, kuunganisha akaunti zako zote au ambazo ziko Benki, pamoja na amana ya muda maalum

(iwe imeiva au la) na akaunti nyingine za aina yoyote ile iwe zinawajibika kwa taarifa au la) na kukata deni au kuhawilisha kiasi chochote kwenye mkopo wa akaunti moja au nyingine au kukamilisha majukumu yoyote au deni lako kwa Benki, kudaiwa huko iwe kwa sasa, baadaye, halisi, kwa pamoja, au kutegemea tukio, ya pamoja au pekee na unaondoa haki za makato deni inayoweza kuwa nazo, kadiri inavyoruhusiwa na sheria. Benki itatoa taarifa kwa Mkopaji baada ya makato.

8.2 Dhamana yoyote iliyowekwa inaweza kuchukuliwa kufidia deni lako lolote kwenye Benki, kwa hiari yake bila kujali kuwa kudaiwa huko kuko katika fedha tofauti na ile ambayo hutumika na Benki kulipa deni.

**9. Gharama**

9.1 Bila kizuizi unaidhinisha Benki kukata akaunti yako ya hundi/ muamala na kufidia ( iwe au isiwe mkopo umetolewa) ada zote za kisheria na gharama nyingine zinazopatikana (pamoja na tozo ya stempu na kodi ya ongezeko la thamani) ambazo Benki inapata kutokana na utendaji au upunguzaji wowote wa dhamana ( kama upo) au utekelezaji au uhifadhi wa Benki wa haki zake chini ya mkataba huu au marekebisho yoyote yanayohusika.

9.2 Utalipa ada, gharama na tozo zote zinazorejewa katika mkataba huu na ada, gharama, tozo na kodi zote ambazo tunaweza kuzipata au kulipa kuhusiana na maandalizi, ukamilishaji au utekelezaji wa mkopo pamoja na:

9.2.1 Gharama za kisheria, tozo, gharama za ukusanyaji na ada nyingine au malipo yanayotokana na ukusanyaji au kujaribu kukusanya malipo yote au sehemu yake pamoja na kodi ya ongezeko la thamani pale inapotakiwa:

9.2.2 Nyongeza yoyote katika ada na gharama kama inavyoamuliwa na kuchapishwa mara kwa mara;

9.2.3 Ada na tozo nyingine zozote zitalipwa kwa mujibu wa kiongozi cha ushuru wa forodha kilichochapishwa na Benki na kurekebishwa mara kwa mara. Kiwango kinachotumika kinaweza kutolewa kwako kwa maombi;

9.2.4 Ada ya kuanzia (ada ya uwezeshaji) ni ada ya mara moja inayotumika kwa mikopo yote, inayotozwa kwa mujibu wa kiongozi cha ushuru wa forodha kinachochapishwa na Benki ambacho kinaweza kubadilika mara kwa mara na kinalipwa kwanza baada ya ithibati ya mwisho ya Benki. Kiwango kinachotumika kinaweza kutolewa kwako kwa maombi;

**10. Kipindi cha Mpito**

Unastahili kipindi cha mpito cha siku kumi(10) mara tu baada ya kutia saini mkataba wa mkopo, alimuradi huchukui pesa hizo. Katika kipindi hicho cha mpito unaweza kuvunja

mkataba wa mkopo bila ya kupewa adhabu yoyote.

**11. Mabadiliko**

Tunaweza kubadilisha, kurekebisha, kuongeza au kufuta masharti haya wakati wowote kwa kukupatia taarifa, isipokuwa kama marekebisho hayo yanasababisha athari hasi kwako. Marekebisho yoyote kwenye maelezo na masharti ya mkataba huu yatafanya tafsiri mpya ya maelezo na msharti ambayo yatakubana wewe na sisi kuanzia tarehe iliyotajwa kwenye taarifa kwa mujibu wa sheria inayohusika.

**12. Majanga asilia (matukio nje ya uwezo wetu**)

Benki haitawajibika kwa kushindwa kutekeleza majukumu yoyote humu yanayotokana na sababu nje ya uwezo wetu moja kwa moja au sio moja kwa moja kutokana na kutenda au kutotenda kwa serikali, mamlaka yoyote ya serikali, fujo, migomo, mapinduzi, vizuizi, uasi wa kiraia, kadari ya Mungu, mabadiliko katika sheria au mabadiliko makubwa katika hali ya soko. Benki itakujulisha mapema kupitia njia mbalimbali, pamoja na ujumbe mfupi(sms) barua pepe, barua au taarifa kwenye ATM, kwenye matawi yetu na njia nyingine ambazo zitakuwa lazima kutumika kwa nyakati tofauti.

**13**. **Utoaji**

Hutakuwa na haki ya kuhawilisha haki, wajibu au maslahi yao yoyote au sehemu yake hapa bila ya ridhaa ya maandishi ya Benki.

**14. Makubaliano ya Jumla**

14.1 Wakati mikopo inapatikana unaahidi kwamba:

14.1.1 Majukumu yako kuhusiana na mikopo nyakati zote sharti yawe japo sawa kwa sawa na majukumu yote ya sasa na baadaye yasiyodhaminiwa;

14.1.2 Mara baada ya kupata taarifa mara moja utaiarifu Benki kuhusu kuwepo kwa shauri lolote la msingi, upatanishi au mwenendo wa kiutawala ambavyo vipo, au kwa kadiri ya uelewa wako, taarifa iliyotolewa dhidi yako ambayo inaweza kutishia uwezo wako wa kutekeleza maelezo au masharti yoyote katika mkataba huu.

14.1.3 Ikiwa kutatokea mabadiliko ya ajira, sharti uiarifu Benki kuhusu mwajiri wako mpya na kuidhinisha uendeleaji wa makato ya mkopo kila mwezi kutoka mshahara wako kupitia mwajiri wako mpya kwa mujibu wa masharti ya mkataba huu.

**15. Anuani na Taarifa**

15.1 Wahusika wanachagua anuani zilizoonyeshwa katika maombi kama anuani za mtaa ambao wewe au sisi kadiri iwavyo watakubali

upokeaji wa taarifa za kisheria). Endapo kila mhusika atataka kubadilisha anuanu yake ya taarifa, mhusika mwingine sharti aarifiwe kwa maandishi, na taarifa hii sharti iwasilishwe kwa mkono au kupelekwa kwa rejesta kwa posta.

15.2 Taarifa nyingine au mawasiliano yote ambayo zinatakiwa au kuruhusiwa kutolewa kuhusiana na masharti ya mkopo huu zitakuwa halali tu zikiwa kwa maandishi na kupelekwa kwa mhusika mwingine au kwa anuani iliyotolewa katika maombi au anuani yoyote iliyobadilika kwa mujibu wa kifungu hiki, isipokuwa nyaraka zozote zitakazotolewa kuhusiana na mienendo ya kisheria mintaarafu mkopo huu zinaweza tu kuwasilishwa kupitia anuani za taarifa za wahusika.

15.3 Taarifa yoyote:

15.3.1 ambayo imepelekwa kwa rejesta ya posta itachukuliwa kwamba imepokewa siku ya 5 (tano) ya biashara baada ya kupostiwa; au

15.3.2 kupelekwa njia ya kawaida itachukuliwa kuwa imepokelewa siku ya 7(saba) ya kazi baada ya kupostiwa; au

15.3.3 kupelekwa kwa mkono itachukuliwa kwamba imepokelewa siku ya kupokelewa.

**Jumla**

16.1 Katika maelezo na masharti haya isipokuwa kama yatakinzana na maudhui, maneno yanayoakisi upekee yatakuwa na maana ya wingi na kinyume chake.

16.2 Kila kipengele cha maelezo na masharti yanaweza kutenganishwa.Ikiwa wakati wowote kipengelee chochote kiko au kinakuwa au kinagundulika kuwa sio halali, haramu, batili au hakitekelezi kwa sababu yoyote na mahakama yenye mamlaka, vipengele vilivyosalia vitaendelea kutumika kikamilifu.

16.3 Mkataba utakaofanywa utakapokubali mkopo utakuwa ndio mkataba wote kati yako na sisi kuhusiana na maudhui ya mkopo. Isipokuwa kama inaelezwa kwa usahili na kukubalika, mabadiliko yoyote kwenye maelezo na masharti ya mkopo huu hayatafanya mkataba mpya.

16.4 Hakuna usumbufu utakaonyeshwa au nyongeza ya muda iliyotolewa na sisi itatumika kama zuio dhidi yetu au msamaha wa haki zetu zozote mpaka iwe imeandikwa kwa maandishi na kutiwa saini na sisi. Hatutabanwa na masharti, wasilisho,udhamini au Ahadi fahamivu au mfumo wake ambao haujaandikwa humu, iwe imeshawishi ukamilishaji wa

mkataba wowote na/au iwe kwa uzembe au la.

16.5 ikiwa siku rasmi ya ulipaji wowote au utozaji wa riba, gharama, ada au tozo haitakuwa siku ya kazi, jambo litashughulikiwa siku ya kwanza ya biashara.

16.6 Utoaji wa kiasi chochote ambacho tunaona kinadaiwa chini ya mkopo unaweza kuwa bila dhamana. Hata hivyo tuna haki ya kumpatia mara kwa mara na baadaye kuhitaji dhamana ikionekana ni lazima.

**17. Taarifa za Siri na Ulinzi wa Data**

**17.1 Katika ibara hii; marejeo kwa:**

17.1.1 **Taarifa Binafsi** ina maana ya taarifa kuhusu mtu halisi anayeweza kutambulika, na pale inapohusika, mtu kisheria, pamoja na, lakini sio pekee, taarifa pia kuhusu: mbari, jinsia, mimba; hali ya kindoa, utaifa, usuli wa kikabila; rangi; usuli wa mazingira ya kijinsia, hali ya kimwili au akili, uwezo kimali, ulemavu, dini, imani; utamaduni; lugha; uzawa, elimu, tiba; fedha, historia ya ajira, namba yoyote ya utambuzi; alama, barua pepe, anuani ya posta au mtaa, mahali; namba yoyote ya utambulisho, barua pepe, namba ya simu, mahali, kitambulisho chochote kingine cha kipekee; kazi nyingine yoyote ya mhusika, taarifa ya kibaiometriki, maoni binafsi, maoni au utashi wa mhusika; msimamo au maoni ya mtu mwingine kuhusu mhusika; mawasiliano yaliyotumwa na mhusika ambayo dhahiri au kiufahamifu yana silka ya kibinafsi au siri au mawasiliano ya ziada ambayo yatafichua mawasiliano ya awali; na jina la mtu linaloonekana na taarifa nyingine binafsi kuhusiana na mtu huyo au kutangaza jina lake pekee kutafichua taarifa ya mtu huyo.

17.1.2 **Mchakato** una maana ya kitendo chochote kinachojiendesha au la kuhusu Taarifa Binafsi, urekebishaji, ukusanyaji, ushauri, ushushaji, uharibifu, utoaji taarifa kwa njia ya usambazaji au kufanya ipatikane kwa namna yoyote, ufuataji, ulinganishaji, upangaji, upokeaji, kurekodi, kuchukua, kuhifadhi, kuboresha, kurekebisha au matumizi ya taarifa. Utumiaji na iliyotumika itakuwa na maana moja.

17.1.3 "**Kikundi**" kinamaanisha Standard Bank Group Limited na kampuni zake tanzu, lakini hakijumuishi Liberty Holdings Limited na kampuni zake tanzu pamoja na vitengo vya kampuni mama yetu kama ilivyokuwa katika Tarehe ya Kuanza Kutumika (Effective Date), na kama itakavyorekebishwa mara kwa mara.

17.2 Unatupa ridhaa kukusanya Taarifa yako Binafsi kutoka kwako na, iwapo ni halali na inafaa , kutoka vyanzo vya umma kuhusu mikopo, udanganyifu na madhumuni yaliyoainishwa hapa chini.

17.3 Iwapo utatupa Taarifa Binafsi kuhusu au kwa niaba ya watu wengine (pamoja na wenye saini katika akaunti, wenye hisa , maafisa watendaji wakuu, wadhamini na wanufaishwa) unathibitisha kwamba unaidhinisha (a) kutupatia Taarifa Binafsi; (b) kuridhia kwa niaba yao kwa utumiaji wa Taarifa zao binafsi hususan upelekaji wowote wa Taarifa ndani au nje ya nchi ambako bidhaa na huduma zinapatikana; na (c) kupokea taarifa binafsi zozote kwa niaba yao.

17.4 Unatupa ridhaa ya kutumia Taarifa yako Binafsi.

17.4.1 Kukupatia bidhaa na huduma kwa mujibu wa mkataba huu na kukupatia bidhaa nyingine na huduma unazoweza kuomba;

17.4.2 Kufanya uchambuzi wa kitakwimu na mwingine ili tuweze kutambua masoko muhimu na mwendo wake, kutathmini na kuboresha biashara yetu (hii inajumlisha kuboresha na kuendeleza bidhaa na biashara mpya);

17.4.3 Kwenye nchi nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambako bidhaa na huduma zinatolewa. Nchi hizi zinaweza zisiwe na sheria sawa za ulinzi wa data kama nchi ambayo bidhaa na huduma zinatolewa. Tunapoweza tutamuomba mhusika anayepokea kuafiki sera zetu binafsi;

17.4.4 Kwa kutumia pamoja Taarifa yako Binafsi na watoaji wetu huduma wengine, ndani na nje ya nchi ambako bidhaa na huduma zinatolewa. Tunaomba watu wanaotoa huduma kwetu Pamoja na watoaji bima wetu kukubali sera zetu iwapo wanahitaji kutumia Taarifa Binafsi yoyote kufanya shughuli zao; na

17.4.5 Ndani ya Kundi.

17.5 Unatambua kuwa tunatakiwa na sheria mbalimbali kukusanya sehemu ya Taarifa yako Binafsi na unaridhia kutumia taarifa hii na sisi:

(i) Utapata taratibu za utumiaji wetu katika maelezo ya Kundi na yetu binafsi. Maelezo haya yanapatikana katika tovuti ya Kundi au kwa maombi.

(ii) Ikiwa huna hakika na hali ya kodi au sheria kwa kuwa Taarifa yako Binafsi inatumika katika nchi mbali na unayoishi, pata ushauri binafsi.

**18. Utafutaji Masoko**

(I) Hapa unaridhia kwa Benki kutumia data na taarifa yako ya siri ndani ya Kundi iwapo ni lazima kwa madhumuni ya utoaji huduma kwako.

(ii) Tunaweza kutumia Taarifa yako Binafsi kukueleza kuhusu bidhaa, huduma na ofa maalumu kutoka kwetu au kampuni ambazo zitaweza kukuvutia. Tutafanya hivi kupitia baruapepe, ujumbe wa maandishi (SMS), mitandao ya kijamii au kukuarifu kwenye maombi yako ya simu ya kiganjani. Iwapo baadaye unaona hutaki sisi kufanya hivi, tafadhali wasiliana nasi kupitia mtandao wetu wa huduma kwa wateja kusitisha huduma hii.

**19. Sheria Inayotumika na Mamlaka**

Mkataba huu wa mkopo utasimamiwa na kutafsiriwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania na Mahakama ya Tanzania yatakuwa na mamlaka ya kutatua migogoro yoyote inayoweza kutokana nayo bila kuathiri haki ya kipekee ya benki kufungua mashauri dhidi yako kwenye mamlaka nyingine yoyote.

**20. Kipengee cha Ridhaa ya Mkopaji**

20.1 Kwa kukubali mkataba wa mkopo huu,Ofisi ya Taarifa za Mikopo (CRB), Mkopaji anakubali na kuiruhusu Benki;

20.1.1 kufanya uchunguzi kutoka benki yoyote, asasi ya kifedha, Chama cha Benki cha Tanzania(“CRB”) TBA kilichopewa leseni na Benki Kuu ya Tanzania kuthibitisha taarifa yoyote iliyotolewa na Mkopaji.

20.1.2 kutafuta taarifa kutoka Benki yoyote, asasi ya fedha na TBA,CRB wakati wa kutathmini akaunti ya Mkopaji.

20.1.3 Kufichua kwa TBA, CRB, benki yoyote na asasi ya fedha taarifa yoyote kuhusu akaunti za Mkopaji zinazohifadhiwa na benki zitapoulizwa;

20.1.4 kutoa taarifa kwa TBA na/au CRB taarifa zote kuhusiana na akaunti zilizopo katika Benki baada ya ukiukaji na/au wakati wa kesi mahakamani;

20.2 Bila kuathiri ujumla wa aya zilizopita, Mkopaji anashauriwa kuelewa maudhui ya Kanuni za Ofisi ya Taarifa za Mikopo za 2012 (GN Na.416 ya 2012 kadiri zitakavyorekebishwa mara kwa mara) kuhusiana na aya ya 20 (Kipengele cha Ridhaa ya Mkopaji)

20.3 Mkopaji ana haki ya-

20.3.1 kujua aina ya taarifa itakayotolewa au kutolewa katika mfumo rejea wa mkopo.

20.3.2 kujua ripoti zao za mkopo

20.3.3 kuomba nakala ya bure ya taarifa yao ya mkopo mara moja kila miezi kumi na mbili, na

20.3.4 kupitia taarifa iliyopo kwenye ripoti ya mkopo.

20.4 Unakubali bila kipingamizi, kwa Benki kuwasiliama moja kwa moja na muajiri wako yeyote wa sasa au

baadaye kuhusiana na usimamizi na ulipaji wa mkopo.

**21 Haki ya kufikisha Malalamiko Benki na kupeleka Benki Kuu ya Tanzania malalamiko ambayo hayakutatuliwa**

21.1 Utaratibu wa kufikisha malalamiko unaweza kupatikana kwenye tovuti ya Benki na matawi mengine yoyote ya Benki.

21.2 Kuifanya iwe ya ufanisi kadiri inavyowezekana, zifuatazo ni njia za kupeleka malalamiko kuhakikisha yanasikilizwa:

(i) Tembelea tawi lolote la Benki na zungumza na mfanyakazi wake;

(ii) Wasilisha malalamiko yako mtandaoni kwa tanzaniaccc@stanbic.com.

(iii) Piga Kituo cha Mawasilano na Wateja namba ya bure 0800 751111 au;

(iv) Weka malalamiko yako kwa maandishi na yatume kwa posta kwenda:

Meneja CCC
Benki ya Stanbic Tanzania Limited
Kituo cha Stanbic
Kitalu 99A
Kona ya Ali Hassan Mwinyi/ Barabara ya Kinondoni
SLP 72647
Dar es Salaam

21.3 Iwapo malalamiko yako hayatatatuliwa ndani ya muda muafaka kwa kutatua malalamiko ya wateja kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya Benki ya Tanzania kuhusu Kinga ya Watumiaji Fedha, unaweza kupeleka malalamiko yako Benki ya Tanzania kwa maandishi kwa:

Benki ya Tanzania
Dawati la Utatuzi wa Malalamiko
Ofisi ya Katibu wa Benki
2 Mtaa Mirambo
S.L.P 11884
Dar es Salaam